

## KIGANO CHA KALE

T.S.Y.. Sengo (Mwanafunzi wa Maisha)

Hapo zamani za kale, kale za utangutangu  
Paliishipo kivele, "kivele wewé ni wangu"  
Wakakaa kama pale, pale penye pingupingu  
Waketi kinyelenyele, kinyelenyele cha nungu  
Lengo ni kufanya kile, kile cha kukata pingu  
Pingu pingitile pingu, kwa nungu na msumeno.

"Kwa nungu na msumeno, pingiti liwe mapingu  
Tuachane na maneno, tuzalishie mafungu"  
Kwisha hicho.kijineno, kijineno cha mipangu  
Ilianza kazi nono, nono kumshinda changu  
"Wewe bwana shika kuno, kuno kama vile kwangu  
Tuishize ndima hii, tusogee twende mbele".

Tusogee twende mbele, mbele kunako uzima  
Mwenyecho kihelehele, moto ule kauzima  
Gogo kalitoa pale, chini likenda kuzama  
Mwenzi kaita "Kivele!", iwapi haki ya umma?  
Mwili ujaa upele, kauli hakuisema  
Mwenziwe anayo hina, ye ye kaishika inda.

Yeye kaishika inda, kengia nayo jikoni  
Mafiga akayapanda, chungu kaweka mékoni  
Chakula akakiranda, kala na wake mezani  
Moto akaufurunda, vipikio aridhini  
Kwishapo akayanena, haya nawe ukapike.

Haya nawe ukapike, ushike na msumeno  
Kihele kibaki peke, niazé si mfanano,  
Watazamaji pwekeke, mezama wauma meno  
wamsaili kivele, ni wewe ufanya vino?  
Jawabu ni tahayuri, kwa buyule kupasuka.

Kwa buyule kupasuka, vipande kutapakana  
Mkweli kapawa shoka, kazize na zote zana  
Watwote kimshika, wamba ni hivyo kazana  
Hakuna kilomwagika, si usiku si mchana  
Na ngano isila hano, Nyoka pigapo nyengine.